*KIZIDUO*

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 15/11/2021

**KUMB.NA.CDC/FUM/61/2021 MAHUDHURIO**

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Bosco S. Mwanginde | Mwenyekiti wa Halmashauri | Mwenyekit |
| 2. | Mh. Ramadhan A. Shumbi | M/M/Kiti wa Halmashauri | Mjumbe |
| 3. | Mh. Christopher N. Mchaphu | Diwani Kata ya Kambikatoto | Mjumbe |
| 4. | Mh. Tusalimu S. Mwaijande | Diwani Kata ya Lualaje | Mjumbe |
| 5. | Mh. Kasimu Y. Haule | Diwani Kata ya Makongolosi | Mjumbe |
| 6. | Mh. Junjulu N. Mhewa | Diwani Kata ya Sangambi | Mjumbe |
| 7. | Mh. Rehema K. Mwamakula | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 8. | Mh. Sophia S. Mwanauta | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |

**B: WATAALAMU**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Tamim H. Kambona | Mkurugenzi Mtendaji | (W) | Katibı |
| 2. | Bw. John F. Maholani | Afisa Utumishi | (W) | |
| 3. | Bibi. Tabu T. Gavu | Kaimu Afisa Mipango | (W) | |
| 4. | Bw. Paul E. Lugodisha | K/Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika | (W) | |
| 5. | Bi. Simphorose A. Kavishe | K/Afisa Ardhi,Maliasili Na Utalii | (W) | |
| 6. | Bw. Nicholaus S. Chambala | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi | (W) | |
| 7. | Bw. Vincent M. Msolla | Afisa Maendeleo ya Jamii | (W) | |
| 8. | Bw. Yohana L. Ngulukia | Afisa Mazingira | (W) | |
| 9. | Bw. Hebel G. Kibona | Afisa Elimu Sekondari | (W) | |
| 10. | Bw. Hubert G. Matungwa | Mkaguzi wa Ndani | (W) | |
| 11. | Bibi. Salome P. Lyimo | Afisa Ugavi na Manunuzi | (W) | |
| 12. | Bi. Rehema P. Mwabulambo | Kaimu Afisa Nyuki | (W) | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | Adv. Athuman M. Bamba | Mwanasheria | (W) |
| 14. | Bw. Happygod Mollel | Kaimu Afisa TEHAMA | (W) |
| 15. | Bw. Simon P. Mbella | Kaimu Afisa Uchaguzi | (W) |
| 16. | Bw. Linus J. Mwanitega | Afisa Mtendaji Mkuu M/M/M | |
| 17. | Bw. Erick F. Nyoni | Afisa Tarafa Kiwanja | |
| 18. | Bw. Kassim A. Kirondomara | Afisa Tarafa Kipembawe | |

**C: WAKARIBISHWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Michombero Anakleth | Katibu Tawala | (W) |

**D: SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bibi. Simbabile O. Mbonile | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Bw. Robert L. Mfugale | Mwandishi wa Vikao |
| 3. | Bibi. Lucy D. Leza | Mwangalizi wa Ofisi |
| 4. | Bibi. Rehema A. Killah | Msaidizi wa Ofisi |

**KUMB.NA.CDC/FUM/62/2021 WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

Mh. Masache N. Kasaka - Mbunge - Kwa taarifa.

**KUMB.NA.CDC/FUM/63/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mheshimiwa Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalamu kwa mahudhurio yao katika kikao. Akawajulisha kuwa ni kikao cha kawaida cha mwezi Oktoba, 2021. Akawataka kuwa makini kujadili agenda za kikao zilizokuwa mbele yao. Kisha akafungua kikao saa 5:06 asubuhi.

**KUMB.NA.CDC/FUM/64/2021 KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda za kikao kama zinavyo onekana hapa chini;-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha Tarehe 15/10/2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha Tarehe 15/10/2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Oktoba, 2021.

6. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Oktoba, 2021.
7. Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa Kipindi cha Robo ya Kwanza, 2021/2022
8. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka, 2021/2022
9. mapendekezo ya matumizi YA Kifungu 0000000/203/4946/DD7/DD7711/2/00000/10A/22019101 Chenye Kiasi Cha Tsh. 120,000,000/= cha Kuendeleza Ujenzi wa Jengo la Utawala Kitumike Kwenye Ujenzi wa Soko la Madini na Kusaidia Ujenzi wa Miundombinu ya Elimu na Afya.
10. Ombi la Kuhamisha Fedha Kwenda Maeneo Maeneo Mengine
11. Mapendekezo ya Kukodisha Kifaa cha Kupima Ardhi (Differential GPS)
12. Ombi la Kumwongeza Mwalimu Bertha M. Gerald, Afisa Elimu Vifaa na Takwimu (SLO) Kuwa Mtia Saini Kwenye Akaunti za Shule za Sekondari.
13. Mengineyo
14. Kufunga Kikao.

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuthibitisha agenda za kikao. Wajumbe walikubali kuwa, agenda hizo zijadiliwe.

**KUMB.NA.CDC/FUM/70/2021 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 kiasi cha Tsh. 4,894,517,139.58. kati ya hizo, kiasi cha Tsh. 2,612,500,000.00 ni fedha kutoka Serikali Kuu, kiasi cha Tsh. 2,200,000,000.00 fedha za UVIKO - 19, kiasi cha Tsh. 26,400,000.00 ni fedha za EP4R na kiasi cha Tsh. 55,617,139.58 ni fedha za uboreshaji wa miundombinu ya maji.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, aidha walisisitiza kuwa;-

- Wataalamu wawe wanatoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa Madiwani pindi wanapohitaji ufafanuzi.
- Miradi yote inayotekelezwa kwa fedha zilizoletwa na Serikali, isimamiwe kwa ukaribu zaidi ili kuleata tija iliyokusudiwa.
- Mwenyekiti wa Halmashauri na Wataalamu waende Isangawana kuongea na wananchi kwa lengo la kuwaweka sawa kutokana na mkanganyiko uliojitokeza wa sh. 300,000,000.00

Mheshimiwa Mwenyekiti pia alieleza masikitiko yake juu ya tuhuma alizobebeshwa kutokana na sh. 300,000,000.00 za kujengea kituo cha afya Mafyeko kupelekwa Isangawana kuendeleza ujenzi wa kituo cha afya na baadae kurudishwa tena Mafyeko hadi kupelekea kushtakiwa kwenye Chama. Akasisitiza kufuata taratibu katika mambo yote.
Baada ya kujadili wajumbe walipitisha.

**KUMB. NA.CDC/FUM/76/2021 KUFUNGA KIKAO**
Mheshimiwa Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalamu kwa kufanikisha kikao. Akasisitiza utekelezaji wa maazimio ya kikao kwa wakati. Kisha akafunga kikao saa 8:41 alasiri.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................ | ........................ |
| **BW. TAMIM H. KAMBONA** | **MHE. BOSCO S.MWANGINDE** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

...15/11/2021.......
**TAREHE**